# Matukio ya SUA

CHUO KIKUU CHA
SOKOINE CHA KILIMO

Oktoba- Desemba, 2023





# Wahitimu 3,095 watunukiwa Shahada mbalimbali katika Mahafali ya 42, SUA

***Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mhe. Jaji Joseph S. Warioba akimtunuku Shahada ya Uzamili mmoja wa Wahitimu katika Mahafali ya 42 ya Chuo hicho.***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilifanya Mahafali yake ya 42 siku ya Alhamisi 23 Novemba, 2023 ambapo Wahitimu 3,095 kutoka programu 74 wametunukiwa vyeti vya kuhitimu elimu yao ya Chuo Kikuu ambapo jumla ya watunukiwa wanawake ni 1,360 sawa na asilimia 43.9 ya Wahitimu wote na wanaume wakiwa 1,735 huku wakihudhurishwa kwa mara ya kwanza Wahitimu wa kwanza wa Ngazi ya Shahada kutoka Kampasi ya Mizengo Pinda Mkoani Katavi.

Alibainisha hayo Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda wakati akitaja takwimu za Wahitimu katika Mahafali hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Michezo vya Kampasi Kuu ya Edward Moringe ambayo yamehudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Chuo hicho Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba.

Katika takwimu hizo wahitimu 2,811 ni kutoka Shahada za Awali ambapo wanaume ni 1,574 na wanawake 1,237, Shahada za Umahiri wahitimu 56 wanaume 29, na wanawake 27, Stashahada ya Juu ya Elimu wahitimu 2 wote wakiwa ni wanaume, Shahada za Uzamivu 18, wanaume 10 na wanawake 8, wahitimu wa Stashahada 140, wanaume 73 na wanawake 67 vilevile wahitimu 68 wa Astashahada, wanaume 47 na wanawake 21.

Aidha Prof. Chibunda alisema kuna vitu ambavyo Chuo kimeweza kutekeleza tangu kufanyika kwa sherehe ya Mahafali ya 41 ya Chuo chao yaliyofanyika Mei 25, 2023 ikiwemo shughuli za Mafunzo ambazo zimeendelea kufanyika kwa Kampasi zote tatu za Chuo hicho Edward Moringe, Solomon Mahlangu na Kampasi ya Mizengo Pinda Katavi vilevile katika mwaka wa masomo 2023/2024 Chuo kimesajili jumla ya wanafunzi wapya wa Shahada za Awali 5,254 na wanafunzi 195 wa masomo ya Uzamivu.

"Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 16,656 kati yao wanafunzi 15,476 ni wa Shahada za awali na wanafunzi 1,180 hawa ni wa Shahada za Juu, aidha Miradi mipya ya utafiti katika kipindi cha mwezi Mei 2023 hadi sasa Chuo kimepata Miradi mipya 18 ua Utafiti yenye thamani ya shilingi bilioni 3.2", alisema Prof. Chibunda

Prof. Chibunda aliwashukuru wadau pamoja na washirika mbalimbali kwa misaada yao iliyochangia kukifikisha Chuo mahali kilipo huku shukrani zaidi akizipeleka kwa Serikali ya awamu ya sita ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwezesha Chuo chao kwa kulipia gharama muhimu za uendeshaji wa Chuo hicho lakini pia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa msaada na Miongozo ambayo wamekuwa wakikipatia Chuo cha SUA na hivyo kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mohamed Chande Othman aliwakumbusha Wahitimu kuwa maisha Kitaaluma ni mitizamo ya maisha kwa ujumla yanayobadilika kila wakati kutokana na misukumo mbalimbali ya Teknolojia na mazingira hivyo amewaomba Wahitimu hao kubadilika kulingana na mabadiliko hayo na kuyatumia kama fursa ili kuleta maendeleo.

Vilevile aliwataka Wahitimu kutumia vyema fursa walizopewa na Serikali na ambazo zitajitokeza kupitia pro-

***Inaendele uk, 2***

**Ardhi ni Hazina**

programu mbalimbali katika kuwajengea uwezo na kuwawezesha kujiajiri kupitia Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili wakashiriki vyema katika shughuli za ujenzi wa nchi, hata hivyo amewapongeza kwa dhati wahitimu hao kwa mafanikio waliyofikia na kustahili kutunukiwa Tuzo walizofuzu.

"Kwa wale wanafunzi ambao hawajahitimu lakini wanazo ndoto za kuhitimu nawaasa kusoma kwa bidii ili watakapohitimu wawe na weredi wa kutosha katika fani zao kwasababu nisingependa kuona wahitimu wa Chuo hiki chenye historia na uzoefu wa muda mrefu katika kufundisha masomo ya Fani za Kilimo wawe wasiojiamini katika kazi zao za kuhudumia watanzania", alisema Jaji Mstaafu Mohamed Chande.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam Prof. Maulid Mwatawala alisema Chuo kimeendesha program mbalimbali za masomo kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho katika Kampasi zake zote tatu ikiwemo Astashahada 2, Stashahada 6, Shahada za awali 39, Stashahada za Uzamili 2, Shahada za Umahiri 57 na Shahada za Uzamivu.




















# SUA yatia Saini Mkataba na Waziri wa Nchi wa Masuala ya Dunia na Mikakati ya Kidiplomasia wa Nchi ya Romania.

***Rais wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano kati ya Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda na Waziri wa nchi wa Masuala ya Dunia na Mikakati ya Kidiplomasia wa Romania Mhe. Traian Laurentio Hristea, 17 Novemba, 2023 Ikulu, Dar Es Salaam.***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mgeni wake Rais wa Romania Mhe. Klaus Iohannis washuhudia utiaji Saini wa Mikataba ya Ushirikiano ikiwemo Mkataba uliotiwa saini na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda na Waziri wa nchi wa Masuala ya Dunia na Mikakati ya Kidiplomasia wa Romania Mhe. Traian Laurentiu Hristea.

Hafla hiyo ya Utiaji wa Saini Mkataba wa Ushirikiano baini ya Tanzania na nchi ya Romania ilifanyika Novemba 17, 2023 Ikulu Jijini Dar es Salaam.

"Uhusiano wa Romania na Tanzania ulianza May 1964 yaani mwezi mmoja tu baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Romania imekuwa mbia wetu kama Nchi na kama Nchi Mwanachama wa Umoja wa Ulaya hivyo ni dhamira yetu kuendelea kudumisha umoja huu" - Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tumezungumzia wigo wa kuongeza ufadhili wa masomo hususani kwenye fani za Udaktari na Ufamasia, pia katika kudumisha uhusiano, Romania imekubali kwa mwaka huu kutoa nafasi 10 za masomo kwa Watanzania katika maeneo tutakayoyachagua" - Rais Samia Suluhu Hassan.



**Ardhi ni Hazina**



# SUA yaadhimisha Siku ya Udongo Duniani kwa kutoa Elimu kwa Jamii

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kupitia Idara ya Sayansi ya Udongo na Jiolojia imeadhimisha Siku ya Udongo Duniani ambayo huadhimishwa Disemba 5, kila mwaka na kuelimisha makundi mbalimbali ya watu kutoka kwenye jamii inayowazunguka kuhusiana na umuhimu wa kuhifadhi udongo ili kuhakikisha unaendelea kuleta tija kwa maisha ya mamilioni ya watu duniani wanaotegemea chakula kutoka kwenye kilimo.

Dkt. Mawazo Shitindi Mhadhiri toka Ndaki ya Kilimo, Idara ya Sayansi ya Udongo na Jiolojia katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA alisema maudhui ya mwaka huu 2023 ni "Udongo na maji ni chanzo cha uhai" hivyo uwepo wa dunia unategemea uhusiano uliopo baina ya rasilimali muhimu ya udongo na maji kwani zaidi ya asilimia 95 ya chakula duniani inategemea uwepo wa rasilimali hizo mbili.

Alisema Udongo usipotunzwa vizuri uwezo wake wa kufanya kazi ikiwemo kurutubisha mimea kwaajili ya maisha ya viumbe hai ikiwemo binadamu unapungua na si tu kupungua kuna wakati utashindwa kufanya kazi au kufa kabisa hivyo ukifa ina maana maisha ya binadamu pamoja na viumbe hai wengine yanakufa pia kwakuwa yanategemea sana Udongo.

"Mimea inamea kwenye Udongo kwa kupata virutubisho na madini mbalimbali kwenye udongo hivyo sisi binadamu tunakula mazao yatokanayo na hiyo Mimea yenye virutubisho na madini kutoka kwenye huo udongo ukweli ni kwamba sisi hatuna uwezo wa kutengeneza Chakula moja kwa moja bali tunategemea Mimea ambayo inategemea Udongo ili iweze kuishi", alisema Dkt. Shitindi


Aidha Dkt. Shitindi alisema Wanasasayansi pamoja na watumiaji wengine wa udongo wameona ni muhimu kuwepo kwa siku ya udongo ili kukumbushana na kutafakari kuwa udongo unafanya nini kwa maisha ya binadamu na wafanye nini kwaajili ya udongo huo ili kuufanya uwe endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.





**Ardhi ni Hazina**

# TADB Yawashika Mkono Wahitimu Waliofanya Vizuri Kimasomo SUA




***Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo ( wa pili kushoto) , Afisa Rasilimali Watu Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Bi. Jacqueline Minja (wa tatu kushoto), wakikabidhi mfano wa hundi kwa wahitimu bora Kumi (10) wa Chuo Kikuu Cha Kilimo Cha Sokoine (SUA). Wanaoshuhudia kushoto ni Makamu Mkuu wa chuo Prof Raphael Chibunda na kulia ni baadhi ya wafanyakazi wa TADB.***

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewapongeza wahitimu bora wa Chuo Kikuu cha Kilimo Cha Sokoine (SUA) cha Morogoro kwa kuwapatia zawadi ya fedha taslimu shilingi milioni Tano (5). Motisha hiyo ya fedha, imetolewa na TADB kama sehemu ya kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri zaidi kupitia mpango mkakati wake mpya uliozinduliwa mwaka huu.

Akiongea wakati wa hafla ya kutoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri na wafanyakazi katika eneo la utafiti, Afisa Rasilimali Watu Mkuu wa TADB Bi. Jacqueline Minja alisema hatua hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



**Ardhi ni Hazina**



# Wizara ya Kilimo kushirikiana na SUA kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo

***Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Dkt. Hussein Mohamed Omar (kulia) akibadilishana nyaraka na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda mara baada ya kusaini mkataba wa ushirikiano baina ya SUA na Wizara ya Kilimo.***

Katika kufikia malengo ya mwaka 2030 ya kilimo kukua kwa asilimia 10, Wizara ya Kilimo imeingia kwenye makubaliano ya kushirikiana na SUA ili kukuza na kuongeza tija ya kilimo kwa wakulima hapa nchini.

Naibu Katibu Mkuu,Wizara ya Kilimo Dkt. Hussein Mohamed Omar akizungumza katika hafla ya kusaini mkataba huo iliyofanyika Jijini Dodoma Desemba 6, 2023, alisema Wizara imeona ni muhimu kushirikiana na taasisi za elimu zinazotoa mafunzo ya kilimo kama sehemu ya mkakati wa kuinua sekta ya kilimo ili ikue sawa na malengo ya Serikali.

Dkt. Omar, alisema kupitia ushirikiano huo wanategemea kuwa wataweza kuwapata wahitimu wengi ambao baadhi yao watakuwa wanapata ajira ya kudumu na wengine kazi za muda kwenda kutafuta namna bora ya kuzalisha kwa tija.

“Tunafahamu kila mwaka Chuo kama SUA kinazalisha wahitimu wengi ambao tunaona tukitumia maarifa na ujuzi walioupata, wakaenda kwenye kutoa ushauri kwa wakulima wetu wataweza kujua namna ya khivyo uchumi wetu utaweza kukua.”, alisema Dkt. Omar.

Aliongeza kuwa lengo la kushirikiana na taasisi za elimu ni kukuza thamani ya kilimo kwani kilimo kwa miaka mingi kimekuwa uti wa mgongo wa uchumi wa watanzania na kwamba lengo ni kufikia matamanio ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukifanya kilimo kuwa chanzo cha mapato nchini.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda, alisema ushirikiano huo sasa umekuwa rasmi kwani ulikuwepo kwa muda mrefu.

Prof. Chibunda aliongeza kuwa SUA inaendelea kuwaandaa wanafunzi na hata wasio wanafunzi katika Kituo Atamizi ili baadaye wawe na uwezo wa kulima kilimo biashara.

“Chuo chetu tumejipanga kutekeleza makubaliano yaliyopo kwenye huu mkataba, sisi faraja yetu ni kuona tunakuwa chachu ya kukua kwa kilimo hapa nchini” alisema Prof. Chibunda

Ushirikiano wa Wizara ya Kilimo na SUA ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya kuhakikisha kufikia mwaka 2030 kilimo kinakuwa kwa asilimia 10 kutoka nne zilizopo hivi sasa.



# SUA yatekeleza adhma ya Mhe. Rais Samia kwa uchangiaji wa damu kwa hiari



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa ameipongeza Serikali ya wanafunzi ya Chuo hicho kwa kufanya Kampeni ya kuchangia damu, kwa lengo la kutekeleza adhima ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuendelea kuokoa maisha ya wenye uhitaji wa damu nchini.

Akifungua kampeni ya uchangiaji damu ambayo imefanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro Prof. Muhairwa aliwataka wanafunzi kuitikia wito wa viongozi wao wa Serikali ya wanafunzi na kuona umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari kwani ni chachu ya kuokoa maisha ya wahitaji wa damu katika nchi yao hivyo waendelee kutekeleza kampeni hiyo muhimu ili damu ipatikane na ikawe msaada kwa Taifa.

"Niwapongeze sana kwa wazo hili, ni jambo ambalo linaenda kugusa maisha yetu ya kila siku, na Mungu anatuhimiza kuwa watoaji zaidi, sisi (Menejimenti ya SUA) tuko pamoja nanyi na tutaendelea kuwapa ushirikiano mnaohitaji ili malengo yenu yatimie". Alisema Prof. Mhairwa.

Nae Rais wa Serikali ya Wanafunzi SUASO Bw. Abdul-Fatah Ibrahim akizungumza wakati wa uzinduzi huo alisema kuzindua kampeni hiyo ikiwa ni katika kuenzi mawazo wa Rais wa TAHLISO ambayo inalenga wanafunzi wa elimu ya juu kwa vyuo vyote nchini kuwa na utaratibu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha ya binadamu wakiwepo wanaopata majeruhi, wanawake wajawazito na watoto.

Aidha aliongeza kuwa Serikali ya wanafunzi imekusudia kuwa na zoezi hilo mara kwa mara kutokana na uhitaji wa damu uliopo katika vituo mbalimbali vya kutolewa huduma za afya nchini.







# Miradi ya Tafiti inahitaji ushirikiano katika kuongeza Tija na Uzalishaji wa Tafiti zenye ubora- Prof. Kashaigili

*Prof. Japhet Kashaigili Mshindi wa Tuzo ya Mtafiti bora wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa mwaka 2022/2023 akipokea Cheti cha Ushindi kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo.*

Utekelezaji wa Miradi ya Utafiti inayohitaji utaalam ni muhimu ikaandikwa kwa ushirikiano baina ya watafiti mbalimbali wakiwemo wa ndani na nje ya nchi ili kuongeza Tija na uwezekano wa kupata ufadhili zaidi ya hayo ni kufanya Tafiti zitakazo zalisha matokeo bora.

Hayo yalielezwa na Prof. Japhet Kashaigili ambae ni Mratibu wa Utafiti na Machapisho kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Mshindi wa zawadi ya Mtafiti bora wa Chuo kwa mwaka 2022/2023 wakati akizungumza na SUAMEDIA kwenye Mkutano wa Majalisi SUA ambao uliambatana na utoaji wa Tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye masomo yao na watafiti katika Tafiti na kukiletea tija Chuo hicho.

Prof. Kashaigili alisema Mradi ambao ameuleta chuoni hapo unahusu maswala ya Mabadiliko ya Tabianchi na Ustahimilivu katika Nyanda Kavu za Kitropiki kuboresha upatikanaji wa maji Jijini Dodoma hivyo ni mkubwa kwakuwa umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 2.4 ukilinganisha na mingine ambayo ipo.

Aidha Prof. Kashaigili alisema Mradi huo umeweza kuwepo na kuonekana kuleta Tija kutokana na ukubwa wake yote hiyo ni kwasababu ya ushirikiano uliopo katika utekelezaji wa Mradi huo ambao umeshirikisha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi mbalimbali za Uingereza, India na Afrika Magharibi ambapo kwa ujumla zipo Taasisi nane kwaajili ya utekelezaji wa Mradi huo.

"Upataji wa zawadi nikiwa kama Mtafiti bora wa Chuo ambae nimefanya Tafiti au Miradi ambayo imeonekana kukiletea heshima Chuo lakini pia kukiongezea kipato kwangu limekuwa ni jambo la fahari sana kwasababu kuna watafiti wengi hapa chuoni lakini nimeonekana mimi" alisema Prof. Kashaigili

Kwa upande wake Prof. Robinson Mdegela ambaye pia alipata tuzo ya Mtafiti bora wa mwaka 2023 kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya, alisema amefanikiwa kupata tuzo hiyo baada ya kufanya tafiti yenye kugusa maisha ya watanzania ikiwemo kupambana na ongezeko la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa tatizo linalokaribia kuua watu karibu 12500 kwa mwaka kiwango ambacho ni karibu mara 10 ya idadi inayosababishwa na malaria au UKIMWI.

Alisema tangu ameanza kufanya tafiti SUA amefanikiwa kupata miradi zaidi ya 35 na kupeleka chuoni karibu shilingi Bilioni 23 kati ya hizo ameweza kutoa ufadhili kwa wanafunzi katika ngazi ya Uzamivu 57 na Umahiri 79 sambamba na kuchapisha majarida 2500.



**Ardhi ni Hazina**



# Fanyeni kazi kwa maslahi ya Taasisi - Prof. Mahonge

***Prof. Christopher Mahonge akitoa akizungumza na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda (hawaonekani pichani).***

Watumishi wa ngazi zote katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wametakiwa kufanyakazi kwa maslahi ya Taasisi kwani maendeleo ya nchi na mahitaji yao kiuchumi yanategemea uwepo wa Taasisi hiyo.

Akizungumza na watumishi wa Kampasi ya Mazumbai iliyopo mkoani Tanga Mwenyekiti wa Kamati ya Kuthibiti Uadilifu (KKU – SUA) Prof. Christopher Mahonge amesema ili nchi iwe na maendeleo inahitaji kuwa na watumishi wanaojituma katika kazi kwa kuzingatia uadilifu na kuepuka rushwa.

Alisema ni vyema watumishi wakajua na kufahamu utawala bora ambao umebeba mambo mengi ikiwa ni pamoja na uadilifu, uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria, haki bila upendeleo, ushirikishwaji na kuepuka rushwa.

"Uwajibikaji hii ni nguzo muhimu sana, sasa kuna vitu tunavipima kwa uwajibikaji yale majukumu ninayopewa je ninayatekelezaje kufikisha malengo niliyopewa, kwa sababu kuna malengo ambayo tumewekewa kila mtu kwa hiyo uwajibikaji ni muhimu sana" alisema Prof. Mahonge

Akizungumzia ushirikishwaji kazini Prof. Mahonge alisema pamoja na kuwepo viongozi ambao wana utaalamu katika maeneo yao ni muhimu wataalamu wanaohusika katika maeneo yao wakashirikishwa kumshauri kiongozi na si kiongozi kujiamulia tu kwani anaweza kufanya makosa kwa sababu hana utaalamu katika eneo jingine.

"Na ili uwajibikaji uende vizuri hapa tunajua kila mtu katika kitengo chake anatakiwa afanye nini, kuna kuwajibika kwenda juu? mfano pale juu tuna Meneja wetu, kwa hiyo labda mtu anasimamia kitengo fulani wale wafanyakazi wengine wanatoa taarifa kwa mwingine kwa kufuata ngazi mpaka inamfikia Meneja" alisema Prof. Mahonge.

Akizungumzia mafunzo yaliyotolewa na KKU-SUA Meneja wa Kampasi ya Mazumbai Bw. Steven Kingazi alisema semina iliyofanywa na kamati hiyo ni muhimu kwa watumishi na ameiomba menejenti ya SUA kuhakikisha kamati hiyo inaendelea kwenda katika Kampasi zake kutoa mafunzo kwani mafunzo yatawakumbusha watumishi wajibu wao.

Alisema semina hiyo imetoa hamasa na kuwakumbusha watumishi wajibu wa mtumishi wa umma katika kuhakikisha watumishi wanaenenda katika misingi ya utawala bora.

"Hii inatusaidia kuhakikisha sehemu ya kazi kunakuwa na uwazi, kunakuwa na uzingatiaji wa utawala wa sheria na kanuni za utumishi wa umma, sehemu ya kazi inakuwa siyo sehemu ya kuomba au kupokea rushwa lakini pia sehemu ya kazi inakuwa sehemu jumuishi, kila mtu kwa kada yake na elimu yake anatakiwa kusikilizwa na kuhusishwa katika maamuzi" alisema Kingazi.





# SUA FM yaanza uhamasishaji kusikiliza vipindi ikiwemo Sauti ya Tiba

*Msimamizi wa Kituo cha SUA Media Bw. Gerald Lwomile akiongea na wananchi wa mtaa wa Konga Kata ya Kauzeni.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia kituo chake cha habari cha SUA Media kimeanza kufanya uhamasishaji kwa watu kufuatilia matangazo yake ya redio na mitandao yake ya kijamii ili kujua na kupata elimu juu ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, hifadhi ya mazingira na afya.

Akizungumza na wananchi wa mtaa wa Konga, Kata ya Mzinga Manispaa ya Morogoro Oktoba 9, 2023 Bw. Gerald Lwomile ambaye ni Msimamizi wa Kituo cha habari cha SUA Media alisema kuwa lengo la ziara hiyo ya uhamasishaji ni kuijulisha jamii umuhimu wa kufuatilia vipindi mbalimbali vinavyorushwa na redio ya SUA FM 101.1 ikiwa ni pamoja na kipindi kipya cha Sauti ya Tiba.

"Kwa miaka mingi tumekuwa tukiona hali si njema sana kwa wakulima walio wengi hivyo kuonekana kama kilimo hakilipi lakini ukweli ni kuwa kilimo kinalipa endapo tu kitafanyika kitaalam kwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazoambatana na teknolojia za kisasa kuanzia upimaji wa udongo, uandaaji wa shamba, upandaji na uvunaji, na kwa kweli SUA imekuwa ikitoa ushauri kwa wakulima" alisema Lwomile

Bw. Lwomile alisema kupitia redio hiyo msikilizaji anaweza kusikia ushauri mbalimbali unaotolewa na watafiti waliobobea katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira, misitu, wanyapori na afya ujumla.

Alisema SUA FM hivi sasa mbali na kurusha vipindi hivyo lakini imeanzisha kipindi kipya kwa kushirikiana na Taasisi inayofanya utafiti wa Kiuchumi na Jamii 'Economic and Social Research Foundation' na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kipindi kinachowapa fursa watu kujua afya zao na namna ya kujikinga na kupata matibabu sahihi.

Alisema kupitia kipindi hicho SUA FM itakuwa ikiwalika wataalam mbalimbali wa afya na wananchi ili kujadili na kujua afya zao, kipindi hicho hurushwa hewani kupitia masafa ya FM 101.1 kila siku ya Jumamosi saa 3 asubuhi na kurudiwa Jumatano saa 5 asubuhi.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Mzinga Manispaa ya Morogoro Mhe. Salum Mrisho Chunga alisema kuwa wanaishukuru SUA FM kwa kuwakumbuka na kuwatembelea ili kuwaelewesha na kuwaelimisha wananchi nini SUA inafanya lengo likiwa kuwasaidia wakulima kulima kwa tija na kuwaondoa kwenye umasikini hivyo ziara hiyo imekuwa chachu kubwa kwa Kata yao na kuahidi kutengeneza mahusiano ya karibu na mazuri na wataalam kutoka SUA ili waweze kupata elimu ya kutosha kuhusiana na Kilimo.





# Kamati ya Kutathmini Ubora wa Mitaala SUA yapitia Mitaala 111

*Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA chini ya Mradi wa HEET Dkt. Jamal Jumanne akiongea na wanahabari (hawapo pichani) mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa kufanya Tathmini ya Mitaala chuoni.*

Kamati iliyoundwa na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwaajili ya Kufanya Tathmini ya Mitaala chuoni hapo imekutana kwaajili ya kutathmini Ubora wa Mitaala iliyokusanywa kutoka kwenye Idara mbalimbali za Chuo hicho ili kuipitia na kujiridhisha ubora wake kabla ya kupelekwa TCU kwaajili ya kuhakikiwa.

Aliyasema hayo Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA chini ya Mradi wa HEET Dkt. Jamal Jumanne wakati akizungumza na SUAMEDIA kwenye Mkutano huo uliofanyika Ukumbi wa VETA Mikumi Mkoani Morogoro ambapo amesema walipokea Mitaala 111 na Mitaala yote imefanyiwa kazi ikiwemo iliyorudishwa moja kwa moja kuwa Idara zianze upya lakini ipo pia ambayo imepewa Maboresho.

“Napenda kuishukuru timu kwa kazi kubwa waliyoifanya kwakweli kazi haikuwa ndogo kwasababu kuna Mitaala ambayo unakuta Ina kurasa hadi 180 hivyo ni kazi kubwa lakini pia nitoe shukrani kwa Menejiment lakini pia Mradi wa HEET kwa kuwezesha hili zoezi kufanyika kwasababu tumejiridhisha sisi kama wenye Mitaala kabla ya kupeleka TCU kwaajili ya uhakiki”, alisema Dkt. Jamal Jumanne

Kwa upande wake Dkt. Nicholas Mwalukasa Mhadhiri kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari SUA alisema kazi kubwa ambayo wameifanya ni kuangalia namna ambavyo Mitaala imeandaliwa ikiwa kama imekidhi matakwa na vigezo vya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) lakini pia kuangalia kama inakidhi mahitaji ya Wahitimu kuweza kutatua changamoto hivyo wamepitia Mitaala hiyo na wanategemea baada ya hapo itaenda kuwa na ubora zaidi na kuweza kukidhi vigezo hivo.

Naye Dkt. Gaymary Bakari kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya SUA alisema upitiaji wa Mitaala iliyokuwepo na mengine ambayo ni mipya baada ya utekelezaji wa HEET ambao umeweka mahitaji ya Mitaala kwenda na wakati lakini pia ambayo itaendana na Soko la Dunia na itakuwa wezeshi katika kujenga uwezo inafaida kubwa kwakuwa inaenda kuwawezesha wahitimu kutoka chuoni kwao kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa ubora zaidi.



*Picha ya pamoja ya Kamati iliyoundwa na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwaajili ya Kufanya Tathmini ya Mitaala chuoni*

**Ardhi ni Hazina**

# Matumizi ya Akili Bandia kuboresha kilimo nchini




**Kiongozi wa Mradi Mkulima GPT na Mhadhiri Msaidizi SUA kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari Bi.Theofrida Maginga akizungumza na wakulima na wadau wa kilimo.**

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Mradi wa Mkulima GPT chini ya ufadhili wa 'BILL na MELINDA GATES Foundation' imetoa mafunzo kwa wakulima wadogo wadogo wapatao 20 mkoani Morogoro kuhusiana na Mfumo wa Akili Bandia unaotumia lugha ya kiswahili utakaomsaidia mkulima kuweza kupata ushauri kuhusiana na kilimo cha mahindi kwa wakati husika lakini pia kutatua tatizo kwenye shamba lake bila uwepo wa Afisa Ugani.

Alibainisha hayo Kiongozi wa Mradi huo na Mhadhiri Msaidizi SUA kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari Bi.Theofrida Maginga wakati akizungumza na SUAMEDIA kwenye warsha iliyofanyika katika Hoteli ya Morena iliyoko Msamvu mjini Morogoro ambapo amesema Mkulima GPT ni 'Chatbot' inayowasaidia wakulima kupata taarifa ya namna ya kuandaa mashamba vile vile kusimamia mashamba ya kilimo cha mahindi kwa kutumia Akili Bandia ( Artificial intelligence).

Alisema lengo la kutumia Akili Bandia ni kwa sababu ya ukuaji wa teknolojia hivyo wao kama watafiti kutoka SUA wanaangalia namna mbalimbali ambazo wanaweza kutumia teknolojia kuwasaidia wakulima katika kufanya shughuli zao za kila siku japokuwa teknolojia inaweza kutumika si kwenye kilimo pekee bali hata kwenye maswala mbalimbali ya kijamii lakini kwa kuanza Mkulima GPT imelenga kuanza na kilimo cha Mahindi na hapo baadae wataangalia na mazao mengine,

Aidha Theofrida Maginga alisema wameleta Teknolojia hiyo kwa Wakulima ili wawe sehemu ya ukuaji wa teknolojia hiyo ndio maana wamefanya warsha ya kuwafundisha Wakulima hao namna ya kutumia Mkulima GPT ili waweze kuanza kilimo cha kisasa ambacho kinafanyika si kwa kutumia Matrekta pekee lakini pia hata kutumia Akili bandia katika kufanya shughuli za kila siku kwa Mkoa wa Morogoro lakini pia na Tanzania kwa ujumla.

"Nafahamu kuwa sisi sote tunafahamu kuwa teknolojia ni changamoto kwa maeneo ambayo hayafikiki au maeneo ya vijijini sana lakini teknolojia inakuwa na lazima tujifunze kuwa nayo na lazima tutengeneze matokeo ambayo yanaweza kuwasaidia wakulima kutumia hii hivyo basi mkulima anaweza akawa na namba ya simu ya 'WhatsApp' tu na akauliza swali kuhusiana na kilimo cha mahindi kwa kutuma ujumbe maandishi au sauti na moja kwa moja akapata majibu ya maelezo kutokana na swali alilouliza", alisema Bi Theofrida Maginga

Akifungua mafunzo hayo Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Samwel Kabote alisema hatua iliyofikiwa katika matumizi ya Akili Bandia ni kubwa na itawasidia wakulima kupata taarifa kwa wakati.

Alisema Chuo Kikuu cha Sokoine kitaendelea kuhakikisha kinasaidia watafiti wachanga katika kuleta tafiti, ubunifu na teknolojia rafiki kwa wakulima ili ziwe na tija. Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu (SUA) Prof. Esron Karimuribo amesema teknolojia hiyo ni zaidi ya utafiti ni muendelezo wa kuboresha shughuli za

*Inaendele uk, 13*

**Ardhi ni Hazina**

Ugani kwa wakulima nchini ambapo Akili Bandia inatumika kusaidia katika kutoa ushauri wa papo kwa papo na kitu kizuri zaidi Utafiti huo umetumia lugha ya watanzania wengi ambayo ni kiswahili lakini pia imetumia ule mfumo wa 'WhatsApp' ambao watu wengi wameuzoea.

Alisema ili kuboresha matokeo makubwa ya kazi hii taasisi na vyombo husika na maswala yote ya Tehama pamoja na habari ikiwemo TCRA, EGA pamoja na Wizara ya Mawasiliano inabidi waione hii kama huduma muhimu kwa Taifa ikiwezekana yawekwe mazingira rafiki kuanzia bei za vifurushi na upatikanaji wa simu za 'WhatsApp' kwa njia rahisi ili wakulima wengi ambao wanahitaji huduma hiyo kuweza kuwa na nyenzo hizo pamoja na uwezo wa kidedha kuweza kupata huduma hiyo kwa haraka zaidi.

"Kupitia teknolojia hii kuna wakati hata hautahitaji Afisa Ugani katika eneo husika bali Afisa Ugani kiganjani hivyo nitoe rai kwa wakulima kuanza mara moja kutumia teknolojia hiyo ambapo tupo sasa kwenye msimu wa kilimo hivyo natamani kuona mwaka huu huu teknolojia hiyo imeanza kutumika katika kuboresha mazao na tija ya uzalishaji hasa kwa zao la Mahindi", alisema Prof. Esron Karimuribo

Naye Bi. Nia Sifanani ambaye ni Mkulima alisema kuwa mfumo wa Mkulima GPT ni mfumo mzuri ambao utaenda kuwasaidia wao kama wakulima kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili shambani na hata kwenye mazingira mengine hususani katika ufuatiliaji wa mazao hata hivyo ameiomba Serikali pamoja na wadau mbalimbali wa kilimo nchini kuweza kuwasaidia katika upatikanaji wa mtandao kiurahisi hasa kwa wakulima waliopo vijijini.



*Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia Prof. Samwel Kabote akifungua mafunzo.*



*Aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu (SUA) Prof. Esron Karimuribo akizungumza katika mafunzo hayo.*





# SUA ina mchango mkubwa kukuza Uchumi wa Buluu



Imeelezwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (SUA) kupitia kwa wataalam wake wabobezi wa Elimu ya Viumbe maji, ina mchango mkubwa katika kufanikisha ndoto ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini Rais Dk. Hussein Mwinyi kuwainuia wananchi wa visiwa hivyo kiuchumi kupitia matumizi ya rasilimali zilizopo baharini maarufu kama Uchumi wa Buluu.

Hayo yalisemwa na Mwalimu Nahida Yusufu wakati akitoa neno la shukrani mara baada ya ziara yao ya kimafunzo katika Idara mbalimbali za Chuo kikiwemo Kitengo cha Uchumi wa Buluu.

Mwalimu huyo aliongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa na shauku kubwa ya kuwakwamua wananchi kiuchumi kupitia rasilimali za bahari na hivyo kwa kupitia elimu waliyopata SUA, haswa ufugaji wa Samaki kisasa wameona chuo hicho kinatoa elimu ambayo kwa kiasi kikubwa wananchi na hasa wanafunzi wa Zanzibar wanatakiwa kuipata ili kuweza kuelewa namna ya kufaidika na uchumi wa Buluu.

''Kwa mfano kwa sasa sisi Unguja tuna hili suala la Uchumi wa Buluu, kwa vile tunazo rasimali nyingi za bahari sasa moja kwa moja kama elimu hii haswa ya mabwawa ya kisasa ambayo tumeelezwa na wataalam hawa wa SUA tunaweza kufika mbali zaidi kama tutaitumia elimu hii kule kwetu Unguja na hivyo tutakuwa tumeziunga mkono Serikali zetu zote mbili katika juhudi za kuwakwamua wananchi kiuchumi" alisema Mwl. Nahida Yusufu.

Mwanafunzi Rehema Ali Bushiri akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake alisema ziara hiyo imekuwa na manufaa kwao kwa kuwa amekuwa akiisikia SUA kwa muda mrefu kama Chuo Kikuu cha Kilimo kikongwe nchini lakini sasa wamefahamu chuo kilivyo na wamehamasika kuja kusoma chuoni hapo katika siku zijazo baada ya kuhitimu masomo yao na kufaulu vizuri na hatimae kujiunga SUA kwa masomo ya elimu ya juu.

''Tumekuwa tukiisikia SUA kwa muda mrefu kama Chuo kikongwe kwenye Kilimo na hatimaye leo tunafurahi kuwa hapo na hii itatufanya tuongeze bidii katika masomo yetu ili siku moja na sisi tuwe wanafunzi wa chuo hiki kwa masomo ya elimu ya juu na kuweza kuipeleka taaluma hii Zanzibar ili wananchi waweze kufaidika na elimu na haswa elimu ya viumbe wa maji ni muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar" alisema Rehema Bushiri.



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya wanawake ya Ben Bela Pamoja na walimu wao wakifurahia maelezo kutoka kwa wataalam wa SUA wakati wa ziara yao ya kimasomo katika Kitengo cha Uchumi wa Buluu.*

**Ardhi ni Hazina**

# SUA yazindua Dawati la Jinsia Kampasi ya Edward Moringe Sokoine



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia Prof. Samwel Kabote (katikati waliokaa) katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki katika uzinduzi wa Dawati hilo akiwemmo Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi Prof. Geoffrey Karugila(wa kwanza kulia waliokaa).*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimezindua Dawati la Jinsia chuoni hapo ili kutimiza malengo ya serikali ya kupunguza ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii hususani chuoni hapo.

Dawati hilo lilizinduliwa Octoba 10, 2023 na Prof. Samweli Kabote, Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Raphael Chibunda ambapo amesema atafurahi kuona Dawati hilo likiwa chachu ya kuimarisha maendeleo ya Jinsia katika maeneo chuo na yanayozunguka chuo hapo.

Alisema kumekuwa na mambo mengi yanayofanyika katika maeneo hayo na hawayasikii lakini yapo na yanaendelea hivyo amelitaka Dawati hilo kufanya utafiti na kuyaibua mambo ili kuimarisha swala zima la maendeleo ya Jinsia kama sehemu ya Taaluma inayopaswa kuchapishwa katika machapisho ya aina mbalimbali.

"kwa vile tunao Wataalamu waliofunzwa vizuri kwa namna ya kufanya Tafiti watusaidie, wapo wataalam wa Sosholojia lakini wapo wataalam wa masuala ya Jinsia hapa chuoni kwaiyo watusaidie kufanya tafiti mbalimbali ili kuweza kuyaibua yale matatizo ambayo yapo na atuyasikii kwa kushirikiana na kamati yetu pia kwaajili ya kuyafanyia kazi " alisema Prof. Kabote.

Kwa upande wake Prof. Geoffrey Karugila Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi akimuwakilisha Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Utawala na Fedha alisema wanatambua kuwa kila mtu bila kujali jinsia yake anauwezo na mchango wa pekee katika maendeleo ya Taasisi yao hivyo wanakusudia kujenga mazingira ambayo yatawezesha wanajumuiya wote wa SUA kufikia uwezo wao kamili wa kiutendaji bila kujali jinsia zao.

"Zoezi hili linahitaji jitihada zetu za pamoja katika kuhakikisha kuwa kuna fursa sawa za elimu, ufikiaji wa rasilimali na maendeleo binafsi ya kila mwanajumuiya " alisema Prof.Karugila.

Naye Dkt. Sarah Chiwamba Mratibu wa Dawati la Jinsia SUA alisema Dawati hilo limeanzishwa na kuzinduliwa kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na azma yao ni kuhakikisha kuwa SUA panakuwa mahali salama kwaajili ya wanafunzi kujifunza na kufikia malengo yao pamoja na wafanyakazi kufanya kazi kwa ufanisi.





# SUA yasaini Mkataba wa kupata Mtaalam wa Ushauri na Usimamizi Ujenzi Kampasi ya Mizengo Pinda Katavi

***Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala SUA Prof. Amandus Muhairwa (kulia) akisaini mkataba wa kupata Mtaalam wa Ushauri wa Usimamizi wa Ujenzi wa Miundombinu na Kampuni ya Crystal Consultancy .***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimesaini Mkataba wa kupata Mtaalam wa Ushauri wa Usimamizi wa Ujenzi wa Miundombinu na Kampuni ya Crystal Consultancy katika Kampasi ya Mizengo Pinda Mkoani Katavi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Zoezi hilo lilifanyika katika Kampasi ya Edward Moringe Sokoine mkoani Morogoro ambapo limeongozwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala SUA Prof. Amandus Muhairwa kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda.

Akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko SUA, Kaimu Mkuu wa Kitengo Cha Ununuzi na Ugavi SUA Kuruthum Abdallah Ndope amesema kampuni hiyo itaenda kusimamia majengo yanayotarajiwa kujengwa katika Kampasi ya Mizengo Pinda ikiwemo Hosteli, Cafeteria pamoja na Jengo la Utawala.

"Chuo kitaenda kunufaika kwa sababu miundombinu itaenda kuboresha na itasaidia katika kuongeza ufanisi mkubwa wa Chuo, udahili wa wanafunzi utaongezeka na kuleta manufaa makubwa kwa Chuo", alisema Kuruthum Ndope.





**Ardhi ni Hazina**




# Serikali kuwezesha vijana kuongeza tija kwenye kilimo.

*Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Ndg. Gerald Geofrey Mweli akiongea na washiriki wa Kongamano la Miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika lililofanyika SUA Ukumbi wa Multipurpose, Desemba 12, 2023.*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) itahakikisha inaendelea kuwapa nafasi vijana kushiriki kwenye kilimo biashara Pamoja na kutambua fursa za kilimo kulingana na wakati uliopo.

Alibainisha hayo Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Mweli wakati akiwasilisha mada iliyohusu maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Programu ya BBT kwenye Kongamano la Maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika lililoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na kufanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Mjini Morogoro, likibebwa na kauli mbiu ya "Miaka 62 ya Uhuru, Kilimo ni Hazina yetu Vijana, Tunajenga Mustakabali Mpya".

Alisema kutokana na mchango wa kilimo kwenye kuchangia malighafi ya viwandani Serikali ya awamu ya sita imejipanga kuhakikisha Programu ya BBT, vijana wake ambao ni asilima 34 ya watanzania wote wanawezeshwa kushiriki katika Sekta ya Kilimo bila kikwazo chochote ambapo Wizara ya Kilimo iliamua kukaa na wadau mbalimbali ili kujadili njia sahihi ya kupiga hatua kwenye kilimo ikiwemo hoja ya elimu, mikopo na masoko kupitia program hiyo.

Ndg. Mweli alisema jumla ya vijana 688 wanatarajiwa kupatiwa mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo ifikapo Januari 15 mwaka 2024 ambapo hekta 231 za mashamba zitatumika katika shughuli za kilimo huku Serikali ikiadhimia kuongeza ukubwa wa mashamba hadi kufikia hekta milioni moja (1,000,000) vile vile Serikali imetenga shilingi milioni 800 ambapo tayari jumla ya shilingi milioni 200 zimekwishatolewa kwaajili ya upatikanaji wa mitaji katika shughuli za uzalishaji wa kilimo.

Kwa upande wake Prof. Samweli Kabote, Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakati akichangia mada kwenye Kongamano hilo amesema miaka mitano baada ya kupata uhuru Serikali ilikuwa na mpango wa kusimamia Kilimo chenye tija kwa Taifa na kila awamu iliyofuata imekuwa ikiendeleza mipango ya kuboresha Sekta ya Kilimo kwa kuwawezesha wananchi kufanya kilimo chenye tija na mazao ya kutosha.



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Samwel Kabote akitoa mada wakati wa Kongamano la Miaka 62 ya Uhuru lililoandaliwa na TBC 1 na kufanyika SUA Ukumbi wa Multipurpose*

## *Baadhi ya picha wakati wa Kongamano la Miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika lililofanyika SUA Ukumbi wa Multipurpose*



















# Ndaki ya Kilimo yachakata maboresho ya Mitaala

Ndaki ya Kilimo, Idara ya Lishe na Sayansi ya Mlaji imekutana na wadau wakiwemo waajiri kutoka Sekta za Umma na Binafsi katika kikao cha kuboresha na kukuza mitaala katika programu zinazofundishwa na Ndaki hiyo, lengo ni kuona mtaala mpya unagusa mahitaji muhimu ya sasa katika kumuandaa mhitimu bora kwenye hatua mbalimbali za kimasomo.

Akizungumza na na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko SUA, Mkuu wa Idara ya Lishe na Sayansi ya Mlaji Dkt. Hadijah Mbwana mara baada ya kikao hicho amlisema mitaala mitano imepitiwa kwenye kikao hicho cha wadau, akisema kutokana na umuhimu wa kujua mahitaji ya soko la nje, wametoa fursa kwa wadau mbalimbali kutoa maoni yao ili kwenye mchakato wa mwisho wa kuzalisha mitaala hiyo, iwe imegusa kwenye maeneo yote muhimu.

"Idara yetu ina kozi kubwa mbili ambapo moja ni ya Lishe ya Binadamu na Sayansi ya Mlaji (Consumer Studies) kwa hiyo tumeleta wadau kutoka kwenye Sekta zote hizo zinazohusika na kozi zetu ili watusaidie kujua yapi yaongezwe kwenye mitaala hii ili Wanafunzi wapate maarifa hitajika kulingana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia", alisema Dkt. Hadijah.

Alisema Mitaala ambayo wanaiboresha sasa inalenga katika kuwafanya wanafunzi wawe na ujuzi wa kujitegemea wenyewe hivyo kile walichokuwa wanakihitaji zaidi kutoka kwa wadau hao ni mawazo, michango yao katika mapendekezo ya Mitaala yao ambayo kwa upande wao walishakaa na kujadili kile kinachohitajika sehemu iliyobaki ilikuwa ni ya wadau ambao ndio wahusika wakuu katika kupokea kile tulichokizalisha au kukipatia Mafunzo.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe kwenye Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaala, Loitsedi Mlali alisema uboreshaji wa Mitaala SUA vile vile kutunga Mitaala mipya ya maswala ya huduma za lishe ni muhimu kwani hivi sasa kuna uwekezaji mkubwa katika Sekta ya afya, ustawi wa jamii na lishe.

Naye Sarah Makweba, mwanafunzi wa mwaka wa tatu Shahada ya Sayansi ya Mlaji alisema mabadiliko hayo ya Mitaala ni mazuri kwa kuwa ni vyema kuangalia namna ya Dunia inavyoenda ili kuweza kujua zaidi kitu ambacho kinatakiwa kibadilike kuendana na uhalisia.





# SUA yawashirikisha wadau wa nje kuboresha mitaala Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii.



*Wadau wa Misitu, Wanyapori na Utalii wa ndani ya SUA na nje ya Chuo wakiwa wameketi Ukumbi wa Reforest, Morogoro Desemba 15, 2023 wakiboresha mitaala iliyopitiwa kabla ya kupelekwa TCU kwa uthibitisho.*

Ndaki ya Misitu, Wanyapori na Utalii ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na wadau wa nje kama sekta binafsi, Taasisi na Mashirika ya Serikali imepitia na kuboresha mitaala pendekezwa lengo likiwa ni kupata maoni kutoka kwa wadau wanaohusika na mnyororo wa ajira ili kujua ni mahitaji gani wanahitaji kutoka kwa wahitimu wa programu zinazofundishwa katika Ndaki hiyo.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao hicho cha wadau kilichofanyika Ukumbi wa Reforest Desemba 15, 2023, kwa ufadhili wa Mradi wa HEET, Dkt. Greyson Nyamoga, Mkuu wa Idara ya Uchumi, Misitu na Mazingira kwa niaba ya Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyapori na Utalii, alisema baada ya mchakato mrefu wa kushirikisha wadau wa ndani kutoa maoni na kufanya utafiti mdogo kuhusu mahitaji mapya ya mitaala sasa wamefikia hatua ya kushirikisha makundi ya nje ambayo yanashiriki moja kwa moja kuwapokea vijana wanapohitimu masomo yao kwa ngazi mbalimbali.

Dkt. Nyamoga aliongeza kuwa kupitia kikao hicho wanategemea kupokea mapendekezo ya mwisho kutoka kwa wadau hao, maboresho ambayo yatapelekea kupata mitaala itakayopelekwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili kupata Baraka huku mategemeo yakiwa kuanza kutumika mwaka wa masomo 2024/25.

Mkuu wa Idara ya Utalii na Mapumziko Huishi, Prof. John Thomas Mgonja akieleza kuhusu mapitio ya mitaala hiyo alisema jumla ya mitaala mitano imepitiwa ambayo inajumuisha programu mbili ngazi ya shahada, moja ya stashahada, astashahada na programu ya uzamili, aidha ameongeza kuwa wadau kutoka nje wataifanya mitaala kuwa endelevu.

Afisa Wanyapori Mkuu – Kitengo cha Uratibu wa Tafiti na Mafunzo, Wizara ya Maliasili na Utalii Bi. Fransisca Jacob Malembeka alisema katika mambo ambayo ameyatazama kwa umakini katika mitaala hiyo ni namna ya kumuandaa mhitimu mwenye uwezo wa kusuluhisha migogoro pamoja na kujua masuala ya usawa wa kijinsia.

Maoni mbalimbali kutoka kwa sekta binafsi, pamoja na taasisi za Serikali ikiwemo TANAPA na Wizara ya Maliasili na Utalii yametolewa kwa ajili ya utekelezaji.



# SUA mabingwa TUSA 2023




Timu ya Mpira wa Miguu ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo imefanikiwa kutwaa ubingwa wa Mashindano ya Shirikirisho la Vyuo Vikuu Tanzania (TUSA) kwa kukifunga Chuo Kikuu cha Ardhi bao 2-1 katika Mashindano yaliyohitimishwa Jijini Tanga mwezi Desemba, 2023.

***Picha: Timu ya Mpira wa Miguu ya Wanafunzi ya SUA ilipopokelewa kwa kishindo na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa mara baada ya kuwasili na kombe la ushindi viunga vya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo***







**Ardhi ni Hazina**

# SUA yashika nafasi ya nne kati ya Taasisi 57 mashindano ya SHIMMUTA 2023.



Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimefanikwa kushika nafasi ya nne kwenye mchezo wa mpira wa miguu kwa mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) yaliyofanyika Jijini Dodoma kuanzia Novemba 12 na kufikia tamati Novemba 25, 2023.

Kwenye mashindano hayo yaliyoasisiwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere mnamo Mwaka 1967 yalifunguliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb) kwa niaba ya Mlezi wa mashindano hayo Makamu wa Rais Mhe. Philipo Isdor Mpango na kilele chake kuhitimishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Mhe. Rosemary Senyamule.

Katika michezo hiyo, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kiliwakilishwa na Timu ya Watumishi ya Mpira wa Miguu ambayo iliundwa na wachezaji 14 imefanikiwa kushika nafasi ya mshindi wanne kwa mashindano ya mpira wa miguu (football) kati ya taasisi, mashirika 57 ambayo yalishiriki kwa mwaka huu.

Mkuu wa msafara wa timu hiyo kutoka Idara ya Michezo Bw. Ladislaus Lwoga akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko cha SUA juu ya mashindano hayo alieleza kuwa mwaka huu timu hiyo imefanya vizuri kulinganisha na maandalizi makubwa ambayo taasisi nyingine walikuwa nayo.

Bw. Lwoga aliongeza kwa kuipongeza Menejimenti ya Chuo kwa kuendelea kuishika mkono Idara ya Michezo kiuchumi jambo lililosaidia timu kusafiri na kuishi vizuri kwa siku zote 14 Jijini Dodoma mpaka kilele cha michezo hiyo, ambapo pia amewahimiza wachezaji wa timu hiyo kuendeleza michezo kwani mwisho wa SHIMMUTA ya mwaka huu ni maandalizi ya mwaka ujao.

Kwa upande wake, Bw. Nickson Msote, Mwalimu wa Michezo SUA akiongea baada ya SUA kushika nafasi ya nne alisema kama mwalimu alikuwa na matagemeo ya timu yake kufika mbali zaidi kwenye mashindano hayo kutokana na maandalizi ya muda mrefu hata hivyo amesema ufinyu wa kikosi pamoja na majeruhi kwa baadhi ya wachezaji ambao walikuwa wamesafiri na hiyo timu umechangia kupoteza mchezo wa kutafuta mshindi wa tatu dhidi ya Timu ya Shirika la Mzinga kutoka Morogoro.

Mashindano ya Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) hufanyika kila mwaka tangia kuasisiwa kwake mnamo 1967 lengo likiwa kujitangaza kwa taasisi, pamoja na kuziunganisha taasisi kwa minajili ya kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.



# Limetolewa na:


**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**

**S.L.P. 3000 CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA**

**Simu: 255-023-2640006/7/8/9, Direct Line: 255-023-2640018**

**Barua pepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz**


**Ardhi ni Hazina**